

J a r i d a l a

SAUTI YA JIJI

TOLEO MAALUMU



**MAADHIMISHO YA MIAKA 15
YA UHUSIANO WA MIJI DADA
KATI YA JIJI LA DAR ES SALAAM NA
JIJI LA HAMBURG, UJERUMAINI.**





Dar es Salaam, Hamburg zatia saini Hati ya Makubaliano ya kudumisha urafiki

Katika maadhimisho ya Miaka 15 ya Uhusino wa Miji Dada kati ya Jiji la Dar es Salaam na Jiji la Hamburg nchini Ujerumani Julai 1, 2025 Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Bw. Elihuruma Mabelya na Mstahiki Meya wa Jiji la Hamburg, Dkt. Peter Tschentscher, walikubaliana kuendelea kudumisha Uhusiano wa Miji Dada kati ya Jiji la Dar es Salaam na Jiji la Hamburg, ambao umedumu kwa miaka 15 hadi sasa, kwa

kutia saini Hati ya Makubaliano ya kuendeleza uhusiano huo katika kipindi kingine cha miaka mitatu (2025-2028).


Hati hiyo ilitiwa saini katika Jiji la Hamburg na Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Bi. Tabu Shaibu, ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Katibu wa Jiji la Hamburg, Bi. Liv Assman.

Tukio hilo lilishuhudiwa na

Balozi wa Tanzania nchini Ujerumani, Mhe. Iddi Hassan Mwamweta na Balozi Mwakilishi wa Tanzania katika Jiji la Hamburg, Mhe. Petra Hammelmann.

Kabla ya kutia saini hati hiyo, Mhe. Balozi Mwamweta alimuhakikishia Bi. Assman kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Ubalozi wa Tanzania nchini Ujerumani itaendelea kushirikiana na Jiji la Hamburg kufanikisha malengo ya majiji hayo katika uhusiano wao.







Mkurugenzi wa Jiji Dar amshukuru Mstahiki Meya wa Jiji la Hamburg kwa urafiki wa kweli

Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Bw. Elihuruma Mabelya, amemshukuru Mstahiki Meya wa Jiji la Hamburg, Dkt. Peter Tschentscher, kwa urafiki wa kweli na misaada ya Jiji la Hamburg kwa wananchi wa Jiji la Dar es Salaam. Bw. Mabelya ameyasema hayo Julai 1, 2025 katika Hafla ya Maadhimisho ya

Miaka 15 ya Uhusiano wa Miji Dada kati ya Jiji la Dar es Salaam na Jiji la Hamburg iliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Jiji la Hamburg nchini Ujerumani. Katika hotuba yake iliyo-somwa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Bi. Tabu Shaibu, amesema kwamba Jiji la Dar es Salaam lime-ridhishwa na ushirikiano

huo na misaada inayotolewa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, uhifadhi wa misitu na elimu.

Mkurugenzi huyo wa Jiji la Dar es Salaam amemthibitishia Mstahiki Meya wa Jiji la Hamburg kwamba jitihada zinazofanywa na Hamburg zinaelezea wazi nini maana ya urafiki wa kweli na zimesaidia sana katika ustawi wa maisha ya wananchi katika jamii.





“Kwa miaka 15 wananchi katika majiji yetu wamefanya kazi pamoja kuimarisha mshikamano wetu katika maeneo ya utamaduni, elimu na mafunzo, kujengeana uwezo na kujihusisha katika masuala ya maendeleo endelevu. Ushirikiano wetu haujanufaisha taasisi zetu tu, bali umeimarisha zaidi urafiki miongoni mwa wananchi wetu.” amesema Bw. Mabelya.





Balozi Mwamweta: Dar es Salaam imarisheni juhudi za upandaji, utunzaji miti

Balozi wa Tanzania nchini Ujerumani, Mhe. Iddi Hassan Mwamweta, Julai 1, 2025 ametoa wito kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na wana-nchi wa Jiji la Dar es Salaam kuimarisha juhudi za upandaji na utunzaji wa miti kuendelea kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Mhe. Balozi Mwamweta ametoa wito huo wakati wa kikao kilichofanyika kati ya

Seneta Katharina Fegebank kutoka Wizara ya Mazingira ya Jiji la Hamburg nchini Ujerumani na ujumbe wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ulioongozwa na Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Bw. Elihuruma Mabelya, waliofanya ziara nchini Ujerumani kushiriki katika Maadhimisho ya Miaka 15 ya Uhusiano wa Miji Dada kati ya Jiji la Dar es Salaam na Jiji la Hamburg. Mhe. Balozi Mwamweta

amesema Jiji la Hamburg ni mfano mzuri wa kuigwa katika kukabiliiana na mabadiliko ya tabianchi kwa mafanikio iliyoyapata.

“mafanikio ya Jiji la Hamburg yanatokana na watu waliofikiri sana, waliopanga, kutekeleza na kusimamia miradi ya upandaji wa miti hadi Jiji lote leo hii limekuwa la kijani, linapendeza na kuvutia”, alisema Mhe. Balozi Mwamweta.



Aliuelekeza ujumbe wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kutumia fursa za uhusiano huo kujifunza na kuwahamasisha wananchi kupanda miti katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam.

Kwa upande wake Seneta Katharina Fegebank alieleza dhamira ya Jiji la Hamburg la kutaka kuendelea kushirikiana na Jiji la Dar es Salaam katika utekelezaji

miradi ya mazingira na udhibiti wa taka ngumu. “Tunapenda kuendelea kutekeza mradi wa uzalishaji wa mbolea mboji uliopo Mwabepande katika Manispaa ya Kinondoni kwa kutumia takataka kutoka katika masoko,” alisema Seneta Katharina Fegebank akishauri pande zote kuanzisha namna bora ya kufanikisha utekelezaji wa mradi huo ulioanzishwa na kuendeshwa kwa ufadhili wa

Serikali ya Ujerumani.

Mhe. Balozi Mwamweta alimuhakikishia Seneta Katharina Fegebank kwamba Ubalozi wa Tanzania nchini Ujerumani utafuatilia shughuli za utekelezaji wa mradi huo na kufanya mazungumzo na uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Manispaa ya Kinondoni.



“Ninaomba Jiji la Hamburg litusaidie kutoa mafunzo na kuwajengea uwezo watendaji wa Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam ili waweze kuwa na uzoefu na kuimarisha utendaji wao katika sekta ya mazingira kwa kupanda miti kama Hamburg mlivyofanya,”

– Mhe. Balozi Mwamweta






Ziara ya mkurugenzi wa jiji la Dar es salaam katika bustani ya mimea ya jiji la Hamburg, nchini Ujerumani

Wakati wa Maadhimisho ya Miaka 15 ya Uhusiano wa Miji Dada kati ya Jiji la Dar es Salaam na Jiji la Hamburg, Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Bw. Elijuru-ma Mabelya, alitembelea Bustani ya Mimea (Botanical Garden) ya Jiji la Hamburg inayosimamiwa na kuendeshwa na Chuo Kikuu cha Hamburg. Lengo la ziara yake ilikuwa ni kujifunza na kupata uzoefu utakaosaidia kuboresha Bustani ya Mimea ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa kushirikiana na Jiji la Hamburg katika kipindi cha mwaka 2025-2028





PICHA ZA MATUKIO MBALIMBALI



MAADHIMISHO YA MIAKA 15 YA UHUSIANO WA MIJI DADA KATI YA JIJI LA DAR ES SALAAM NA JIJI LA HAMBURG





MAADHIMISHO YA MIAKA 15 YA UHUSIANO WA MIJI DADA KATI YA JIJI LA DAR ES SALAAM NA JIJI LA HAMBURG





Jarida hili limeandaliwea na;
KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI (GCU)
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

S.L.P 20950

1 BARABARA YA MOROGORO
11882 DAR ES SALAAM

SIMU: 0738 378 386

NUKUSHI: 2128800

BARUA PEPE: info@dcc.go.tz

TOVUTI: www.dcc.ho.tz

